East African Journal of Swahili Studies, Volume 5, Issue 2, 2022
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 5, Issue 2, 2022
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Utu wa Wahusika Viumbe wa Kiuhalisiajabu: Mtazamo wa Mwandishi Said Ahmed Mohamed

*Peres Akello Obondo[1*], Dkt. Juliet Akinyi Jagero, PhD[1] & Dkt. Naomi Nzilani Musembi, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga, S. L. P. 210-40601 Bondo, Kenya.
[*] ORCID ID https://orcid.org/0000-0001-6371-9264; Barua pepe ya mawasiliano: perezakellob@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*17 Desemba 2022*

**Istilahi Muhimu**:

*Utu, Uhalisiajabu, Riwaya Mpya na Mhusika.*

**IKISIRI**

Utu ni sifa mojawapo muhimu katika mahusiano mazuri maishani mwa binadamu. Utu huhusisha wema. Utu ni sifa ambayo huhusishwa na wahusika mbalimbali katika dunia halisi na hata kwenye dunia ya fasihi. Wahusika ni muhimu katika fasihi kwa vile kupitia kwao, mwandishi huweza kupitisha ujumbe aliokusudia kwa wasomaji. Wahusika huwa wa aina mbalimbali wakiwemo wahusika wa kiuhalisiajabu ambao pia huchangia katika kupitisha ujumbe wa mwandishi sawia na wahusika wa kihalisia. Tafiti za awali zimewasawiri wahusika binadamu wakionyesha utu kwa sababu ni sifa muhimu anayopaswa kuwa nayo binadamu. Hata hivyo, waandishi wa Kiswahili akiwemo Said A. Mohamed wamesawiri wahusika wa kiuhalisiajabu wakionyesha utu kwa viumbe wengine. Huu ni mtindo ambao umeanza kutumiwa katika riwaya mpya na waandishi wa fasihi ya Kiswahili. Hivyo basi, utafiti huu ulichanganua kiuhakikifu wahusika viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed ili kudhihirisha kwamba hata viumbe wasio binadamu huwa na sifa ya kibinadamu ya utu. Lengo mahususi lililoongoza utafiti huu lilikuwa kufafanua jinsi viumbe wa kiuhalisiajabu wanavyodhihirisha utu katika riwaya za Said A. Mohamed. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya kiuhalisiajabu kama inavyofafanuliwa na Zamora na Wendy (1995). Nadharia hii hueleza matukio katika hali ya kutisha, kushangaza na kuogofya kwa kuziwasilisha kana kwamba ni hali ya kawaida. Eneo la utafiti likiwa fasihi ya Kiswahili, utanzu wa Riwaya. Sampuli ya kimakusudi ilitumika kuteua riwaya tatu za Said A. Mohamed hususan: Babu Alipofufuka (2001), Dunia Yao (2006) na Nyuso za Mwanamke (2010). Data ilikusanywa kutokana na kusoma riwaya hizo tatu zilizoteuliwa na kudondoa sehemu zinazolingana na lengo la utafiti. Data ilidondolewa, ikanukuliwa, ikapangwa kisha kuchanganuliwa. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa kwa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014

kweli viumbe wa kiuhalisiajabu wana sifa za utu kama upendo, ukarimu, kusamehe miongoni mwa mengine.

**APA CITATION**

Obondo, P. A., Jagero, J. A. & Musembi, N. N. (2022). Utu wa Wahusika Viumbe wa Kiuhalisiajabu: Mtazamo wa Mwandishi Said Ahmed Mohamed. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(2), 131-141. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014.

**CHICAGO CITATION**

Obondo, Peres Akello, Juliet Akinyi Jagero and Naomi Nzilani Musembi. 2022. "Utu wa Wahusika Viumbe wa Kiuhalisiajabu: Mtazamo wa Mwandishi Said Ahmed Mohamed". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (2), 131-141. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014.

**HARVARD CITATION**

Obondo, P. A., Jagero, J. A. & Musembi, N. N. (2022) "Utu wa Wahusika Viumbe wa Kiuhalisiajabu: Mtazamo wa Mwandishi Said Ahmed Mohamed", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(2), pp. 131-141. doi: 10.37284/jammk.5.2.1014.

**IEEE CITATION**

P. A. Obondo, J. A. Jagero & N. N. Musembi "Utu wa Wahusika Viumbe wa Kiuhalisiajabu: Mtazamo wa Mwandishi Said Ahmed Mohamed", *EAJSS*, vol. 5, no. 2, pp. 131-141, Dec. 2022.

**MLA CITATION**

Obondo, Peres Akello, Juliet Akinyi Jagero & Naomi Nzilani Musembi. "Utu wa Wahusika Viumbe wa Kiuhalisiajabu: Mtazamo wa Mwandishi Said Ahmed Mohamed". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 2, Dec. 2022, pp. 131-141, doi:10.37284/jammk.5.2.1014.

## UTANGULIZI

Utu ni dhana ambayo inatambulika ulimwenguni kote kwa sababu ya mahusiano ya binadamu kijamii. Utu hukinzana na vita, ukabila, siasa mbaya, uongozi mbaya, utabaka na chochote kile kinachohusisha unyanyasaji wa binadamu (Pietersen, 2005).

Utu hujumuisha upendo na huruma haswa kwa kiumbe na huwa ni muhimu katika maisha ya binadamu. Aidha, utu huendeleza upendo na utangamano baina ya watu. Bila utu, panaweza kuwepo na vita, watu kuteswa, uongozi mbaya na maovu mengine. Kwa mujibu wa Cornevale (2006), binadamu wana mahusiano kupitia kuishi kwao, baada ya kifo na kupitia kwa hisia zao. Cornevale, anaendelea kueleza kuwa, binadamu tu ndiye ana utu kwa sababu za tofauti za hisia zao na zile za wanyama. Watunzi mbalimbali wa kazi za kifasihi wakiwemo E. Kezilahabi kwenye vitabu vyake kama vile *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991), K. Wamitila kwenye riwaya, *Bina- Adamu!* (2002) na *Musaleo! (2004)* na T. Olali katika riwaya zake za *Mafamba* (2008) na *Watu wa Gehenna* (2012) wameendeleza maudhui ya utu, ijapokuwa yamehusisha utu na binadamu. Utu hudhihirika haswa kwa binadamu kwa vile ana hisia na hupenda kutoa usaidizi kwa viumbe wenzake. Ijapokuwa utu huonekana sana kwa binadamu, wanyama na viumbe wengine pia huwa na utu.

Viumbe mbalimbali huhusishwa na uhalisiajabu ikiwemo mizimu, mizuka, miungu, vifaa, binadamu hai, wanyama miongoni mwa viumbe wengine. Mbiti (1980) anaeleza kuwa, Waafrika wanaamini kuna nguvu za ajabu ambazo hutoka kwa kiumbe wa ajabu mwenye nguvu na uwezo zaidi. Kiumbe huyu tena husambaza nguvu zake kwa viumbe wengine au kwa vifaa. Mbiti, anasisitiza kuwa, nguvu hizi za ajabu huweza kutumika kwa njia chanya au hasi. Aidha, anasema kuwa wakristo huamini tu kuwa nguvu hizi zinazotumika na viumbe hawa, hutumika kutenda mambo maovu tu kwa kuwa hudhibitiwa na binadamu kama vile wachawi na waganga. Hivyo, kutokana na mtazamo huu; utafiti uliweza kudhihirisha kuwa viumbe wa kiajabu hawatumiki tu kwa njia hasi bali pia hutumiwa kwa njia chanya.

## UHAKIKI WA MAANDISHI

Uhalisiajabu ni dhana iliyobuniwa na msanii wa Ujerumani, Franz Roh katika kitabu chake *Nach-expressionismus, magischer Realismus* na inahusishwa na waandishi wa Marekani ya Kusini au hata nchi zinazoitwa Ulimwengu wa Tatu na hutambulishwa na sifa mbalimbali. Sifa hizi ni za

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014

kuyaelezea matukio ya kifantasia au ya kiajabu au kichawi kwa namna ya moja kwa moja na kwa namna inayoyofanya yaonekane kama ya kawaida tu. Wamitila (2003) anasema kuwa, mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana.

Akifafanua kuhusu dhana ya uhalisiajabu, Mbatia (2002) anaeleza kuwa ni istilahi inayotumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia. Uhalisiajabu hufanya hivyo kwa kuyaeleza matukio kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Wasanii wanaoutumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokea katika maisha ya kawaida ya jamii inayohusika. Utafiti huu ulidhamiria kubainisha iwapo matukio haya ya kiajabuajabu yalitokea katika maisha ya kawaida ya jamii husika kwenye riwaya teule.

Dhana ya utu ilipata umaarufu kati ya karne ya kumi na nne na kumi na saba (Samba, 2018). Utu ni hali ya kuwa na uadilifu. Utu huhusishwa na matendo mema kama vile: kulisha, kusaidia katika shughuli, kuongoza na hata kutahadharisha wengine kiasi cha kuwaathiri vyema kisaikolojia. Ni uzuri wenye nia ya kutia wengine mazuri na mema. Utu ni kufanya mema unavyotarajiwa na wanajamii (Oruka, 1990). Maelezo haya yana umuhimu kwa utafiti huu kwa vile yanasaidia kubainisha jinsi wahusika wa kiuhalisiajabu hutenda mazuri na mema kwa wenzao.

Watafiti wengi wameshughulikia suala la utu. Baadhi ya watafiti hawa wamelishughulikia suala hili kama mojawapo ya maudhui katika kazi mbalimbali za kifasihi. Waandishi hawa wa awali kama Ndanu (2018 ) na Chepkoech (2018 ) wameshughulikia utu kama kijimada katika kazi zao zenye maudhui tofauti. Aidha wao wamelenga zaidi utu unavyodhihirishwa na binadamu. Licha ya kuwa utu ni sifa ambayo inahusishwa na binadamu, viumbe wengine pia hudhihirisha utu. Katika hali halisi viumbe kama wafu, vivuli, mawe hawawezi kudhihirisha utu. Kutokana na haya, utafiti huu ulishughulikia suala la utu wa wahusika viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed ukiwa na lengo la kubainisha kuwa wana sifa ya utu kama binadamu halisi.

Neno lingine linalohusiana na utu ni Ubuntu. Neno Ubuntu linatokana na dhana “Umuntu” kutokana na lugha ya kizulu ambayo inatafsiriwa kuwa “Mtu ni mtu kwa sababu ya wenzake.” Tutu (2004) anaeleza kuwa, Ubuntu inamaanisha upendo, ukweli, amani, furaha, uzuri, na kuwa na matumaini. Ubuntu ni sifa ya uzuri wa binadamu kwa binadamu mwenzake. Tangia awali, falsafa ya Ubuntu imekuwa ikiwaongoza waafrika. Huonyesha jinsi binadamu hushirikiana na binadamu wengine, mazingira na Mungu muumba. Ni falsafa muhimu kwa binadamu kwa kuwa binadamu bila Ubuntu binadamu huwa mlafi, mwenye majivuno, hujipenda na hata kuwa na tabia ya uzinifu.

Kipengele cha wahusika ni muhimu katika kuunda kazi yoyote ya kifasihi. Kipengele hiki hushirikiana na vipengele vingine vya kifani katika kutoa maudhui ya kazi yoyote ya kifasihi. Kwa kawaida wahusika hujengwa kisanaa na mwandishi ili waweze kuwakilisha dhana mbalimbali za maisha katika jamii (Msokile, 1999). Mwandishi huwajenga wahusika wake kwa kutumia mbinu mbalimbali ili kuwatofautisha na hivyo kuiwezesha hadhira yake kutambua sifa au tabia za mhusika fulani zinazomtofautisha na mhusika mwingine katika kazi husika.Hata hivyo, ni vema ifahamike kuwa kila msanii wa kazi ya kifasihi ana mbinu zake za kuwajenga wahusika wake. Hii ina maana kuwa, msanii wa kazi ya kifasihi anaweza kutumia mbinu moja au zaidi katika kazi fulani kwa kutegemea aina ya utanzu anaoushughulikia. Utafiti huu unaonyesha namna wahusika wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed wanvyodhihirisha sifa ya utu.

## MISINGI YA UTEUZI WA MADA

Kuna tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu uhalisiajabu. Watafiti wamezishughulikia katika viwango tofauti. Baadhi ya tafiti hizo ni ule uliofanywa na Walibora (2010), Vutagwa (2013), Mwangi (2013) , Magaju (2004) na wengineo. Kazi hizi aghalabu, zimeangazia kwa jumla suala la uhalisiajabu. Watafiti hawa wamezungumzia sifa za uhalisiajabu, tofauti ya uhalisiajabu na uhalisia na matukio yalivyodhihirika katika vitabu tofauti. Utafiti pia umefanywa kuhusiana na utu ila tu ni

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014

suala ambalo limeshughulikwa tu kwa kifupi chini ya mada nyingine. Ndanu (2018) ameshughulikia suala la utu katika *Maudhui ya Ukombozi katika Wimbo Mpya na Msururu wa Usaliti.* ameangazia utu kama maudhui katika kazi yake ya *Itikadi katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed.* Chepkoech (2018) naye anazungumzia suala la utu katika *Usawiri wa maudhui yenye kufunza wanafunzi wa vyuo maadili mema: Tathmini ya Alidhani Kapata na Damu Nyeusi.* Tofauti na tafiti hizi, utafiti huu ulishughulikia suala la utu wa wahusika, viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya za *Babu Alipofufuka* (2001)*, Dunia yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke (*2010) za Said A. Mohamed lengo likiwa ni kubainisha kuwa, wahusika hawa wanamiliki sifa ya utu inayohusishwa na binadamu pekee. Uhakiki hutegemea mabadiliko ya kijamii kulingana na wakati na katika maendeleo ya kihistoria ambayo kwa njia moja au nyingine huathiri maendeleo ya fasihi. Pia, hakuna uhakiki unaoweza kudaiwa kwamba umekamilika kwa sababu wahakiki labda hutofautiana kwa mitazamo na misimamo (Wamitila, 2010). Utafiti huu ulishughulikia suala la uhalisiajabu ili kudhihirisha mabadiliko ya mtazamo kuwa viumbe wa uhalisiajabu hudhihirisha uovu (Mbiti, 1980).

## MISINGI YA KINADHARIA

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisiajabu. Zamora na Wendy (1995) wanatueleza kwamba nadharia hii iliasisiwa mwaka wa 1925 na Mjerumani aliyejulikana kama Franz Roh aliyekuwa mhakiki wa sanaa. Franz Roh alitumia istilahi uhalisiajabu katika muktadha wa sanaa kuelezea na kuonyesha jinsi ya kusawiri aina fulani ya uujiza uliomo kwenye uhalisi uliozoelewa na unaotokana na ujarabati.

Zamora na Wendy (1995) wanatueleza kwamba nadharia hii pia hujulikana kama nadharia ya uhalisia mazingaombwe na ni mojawapo ya nadharia za usasa leo ambazo hushikilia kwamba kazi ya fasihi hujengwa kutokana na kuchanganya mambo ya kiuhalisia na mambo yasiyo ya kiuhalisia. Nadharia hii imeweza kuendelezwa na wataalamu wengi kama;

Njogu & Chimerah (1999) wanaeleza kuwa, uhalisiajabu ni nadharia ambayo inakiuka sifa za uhalisia kama zilivyozoelewa na waandishi wa karne ya kumi na tisa na ishirini. Katika uhalisiajabu, matukio yasiyoaminika husawiriwa. Mambo ya kiajabu yanaelezwa kwa namna ya moja kwa moja na kuonekana kuwa ya kawaida. Hali ya kushangaza na kuogofya huwasilishwa kuwa ya kawaida katika uhalisiajabu; ndoto na uhalisi vinachanganywa.

Nadharia mwafaka katika uchambuzi wa kazi hii kwa sababu kuna matukio yasiyoaminika ya kifantasia, yanasawiriwa kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni ya kawaida katika riwaya hizi. Vilevile mambo ya kiajabu yanaelekezwa kwa namna ya moja kwa moja kana kwamba ni ya kawaida.

Nadharia hii ina mihimili yake ambayo imetokana na kazi za Danow (1995), Cooper (1998), Zamora na Wendy (1995) na Encarta encyclopaedia (2002). Wanauhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika mazingira finyu, hivi huvuka mipaka ya kitaifa au kimataifa. Wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa. Vilevile, mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiajabu. Hivyo, utafiti huu uliongozwa na mihimili ifuatayo:

Mhimili wa kwanza; Katika nadharia ya uhalisiajabu, ndoto huchukua nafasi muhimu sana kwani matukio mengi hutokea wakati mtu anapolala au yumo mawazoni. Uhalisi na ndoto vinachanganyika. Hakuna mipaka ya uhalisi na ndoto katika uhalisiajabu. Labda wakati mtu anapoota ndipo yupo uhalisini na wakati yupo uhalisini ndipo yumo ndotoni. Malcolm (1959) anaeleza kuwa, ndoto ni mtiririko wa mawazo ya ndani ya mtu aliye macho au anayelala yanayoambatana na maono, taswira za matukio, mazingaombwe, fikira za uwongo, udhanifu, ndoto za mchana, ukisiaji, uwepo na malengo, matarajio na matamanio. Kwa kuwa ndoto huchukua nafasi muhimu katika nadharia ya uhalisiajabu, utafiti ulichunguza jinsi mwandishi Mohamed ametumia ndoto katika riwaya zake kufanikisha ujumbe wake.

Mhimili wa pili; Matukio hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Jambo hili hufanywa kwa kutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili. Mwandishi hutumia mbinu rejeshi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014

kuvunja mtiririko wa vitushi (Zamora & Wendy, 1995). Utafiti huu pia uliweza kurejelea matukio rejeshi katika riwaya za Said A. Mohamed ili kuweza kuthibitisha iwapo kuna ukosefu wa mantiki.

Mhimili wa tatu; Simulizi zote hutegemea uhalisia ambapo kazi za fasihi za uhalisiajabu husimulia mambo ya kiajabuajabu na ya kutisha kwa namna ya uhalisia na ukawaida. Hivi, katika matini ya uhalisiajabu, jambo lolote huweza kujiri wakati wowote. Mathalani, mtu aliyelala ndani anaweza kujikuta yuko nje asubuhi. Matokeo haya ya kiajabuajabu huonekana kuwa ya kawaida, pia huwa na hali za kushangaza, kuduwaza na kuogofya (Zamora & Wendy, 1995). Mwandishi huyu anatukumbusha kuwa, pamoja na kuwa tunaishi maisha ya kawaida yapo upande wa pili yaliyosheheni wazimu na maajabu. Kwa kuwa matokeo ya kiajabuajabu huonekana kuwa ya kawaida, hushangaza, huduwaza na huogofya, utafiti huu ulichanganua matokeo haya ya kiajabuajabu yalivyo katika riwaya za Said A. Mohamed.

Mhimili wa nne; Mazingira ni sehemu muhimu katika aina hii ya fasihi. Wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa. Vilevile, mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiajabu (Zamora & Wendy, 1995). Hivyo, utafiti huu pia ulinuia kurejelea mazingira na kutambulisha uajabu katika mazingira mbalimbali yalivyojitokeza kwenye riwaya za Said A. Mohamed kuafikisha mada na malengo ya utafiti.

Mhimili wa tano; Fantasia au uhalisiajabu hutumia taswira kujengea msomaji picha mawazoni mwake na kumwezesha kutafakari kuhusu matukio hayo yanayotokea. Hii inatokana na ukweli kuwa kazi ya fasihi husawiri maisha halisi ya binadamu kupitia lugha ya picha na ishara kisha kuiwakilisha katika jamii. (Malcom, 1959).

Mihimili mitano iliyoelezwa hapa inawasilisha mawazo katika nadharia ya uhalisiajabu yaliyoongoza uchunguzi wa utu wa wahusika viumbe wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed.

**Eneo la Utafiti**

Eneo la utafiti huu ni fasihi ya Kiswahili, utanzu wa riwaya. Utafiti huu ulihusisha utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu. Utafiti ulilenga riwaya teule za Said A. Mohamed ambazo ni: *Babu Alipofufuka (2001)*, *Dunia Yao (2006)* na *Nyuso za Mwanamke (*2010). Aidha, mtafiti alisoma kazi mbalimbali kuhusiana na nadharia iliyotumiwa katika kuchanganua data. Maandishi mbalimbali yalisomwa maktabani ikiwa ni pamoja na tasnifu, majarida, makala na magazeti ili kupata data faafu ya mada ya utafiti. Mtandao pia ulitumiwa katika harakati za utafiti huu ili kupata data toshelevu kuhusiana na mada ya utafiti.

**Usampuli na Usampulishaji**

Ameandika vitabu vingi vikiwemo riwaya, tamthilia na ushairi. Riwaya zake ni kama vile: *Kiza Katika Nuru* (1988), *Asa1i Chungu* (1977), *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Tata za Asumini* (1990), *Kiu* (1972), *Nyota ya Rehema* (1976), *Kivuli Kinaishi* (1990), *Amezidi* (1995), *Sadiki Ukipenda* (2002), *Mhanga Nafsi Yangu* (2012) na *Makadume* (2013). Kazi zake za Ushairi ni kama vile: *Sikate Tamaa* (1980), *Kina cha Maisha* (1984) na *Jicho la Ndani* (2002). Ameandika tamthilia kama vile: *Pungwa* (1988), *Posa za Bi. Kisiwa* (2007), *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2004), na *Mashetani Wamerudi* (2013). Pia, ana mikusanyiko nyingi ya fasihi simulizi kama vile, *Vito vya Hekima*, *Gharama ya Amani* (2014) *Semi na Maneno ya Mshangao* (1974) na *Semi*, *Milio na Tashbihi* (1981). Usampulishaji wa kimakusudi ulitumika kuteua mwandishi pamoja na vitabu vyake. Mbinu hii ilitumika kuteua riwaya hizi teule za mwandishi Said A. Mohamed kwa kuwa, kati ya waandishi ambao wameendeleza maudhui ya utu, Said A. Mohamed ameendeleza maudhui ya utu kupitia viumbe ambao si binadamu ambao kwa kawaida huwa hawadhihirishi utu. Mbinu hii ya usampulishaji pia ilitumika kuteua riwaya kwa kuwa uhusika hujidhihirisha wazi kwenye riwaya. Sampuli ya kimakusudi ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huichagua huku akiwa na matarajio kuwa itawakilisha kundi lengwa. Hivyo, riwaya za Said A. Mohamed zilizoteuliwa ni *Babu Alipofufuka* (2001), *Nyuso za Mwanamke* (2010) na *Dunia Yao* (2006).

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014

**Mbinu za Ukusanyaji Data**

Data zilikusanywa maktabani kwa kudurusu na kuchanganuliwa kwa riwaya tatu za Said A. Mohamed; *Babu Alipofufuka (2001), Dunia Yao (2006) na Nyuso za Mwanamke (*2010). Usomaji wa kina ulifanywa kwa majarida na machapisho yalioandikwa kuhusiana na mada ya utafiti, utafiti na mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu. Aidha, palikuwepo na usomaji wa vitabu vya wataalamu mbalimbali vinavyotaja mambo ya utu ili kupata uelewa zaidi kuhusu dhana hiyo. Tasnifu zilizohusiana na mada ya utafiti pia zilipitiwa kwa kuongozwa na utafiti katika ukusanyaji wa data. Barua, nyaraka na taarifa mbalimbali zilizopo katika mtandao na wavuti pia zilitumika ili kupata data faafu. Kwa kutumia mbinu hizi, mtafiti aliweza kubainisha vipengele mbalimbali vya utu wa wahusika viumbe wa kiuhalisiajabu. Data faafu zilidondolewa kutoka kwenye machapisho na maandiko haya na kunakiliwa kwa kurejelea malengo ya utafiti.

**Uchanganuzi na Uwasilishaji Data**

Uchanganuzi ulilenga utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu. Data iliyokusanywa ilinukuliwa, ikapangwa na kisha kuchanganuliwa ili kuafiki utafiti. Mtafiti alichanganua jinsi katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010) katika mkabala wa nadharia ya Uhalisiajabu. Mifano mbalimbali katika riwaya teule za Said A. Mohamed ilitumiwa kudhihirisha matumizi ya uhalisiajabu kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia. Matukio ya utu yalisawiriwa na kuelezwa bayana kwa kufuata hatua zifuatazo, kudondoa sehemu matukio ya utu yamesawiriwa, kuonyesha umbo wanalochukua wahusika viumbe wakionyesha utu na kuonyesha athari ya utu kwa wahusika binadamu katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010). Data iliyokusanywa iliwasilishwa kwa njia ya maelezo na maandishi. Pia, mifano yenye kunukuu sehemu za riwaya ya kubainisha ujumbe husika ilitolewa baada ya usomaji wa kina, kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu iliyoongoza utafiti huu.

**UDHIHIRISHAJI WA UTU WA VIUMBE WA KIUHALISIAJABU KATIKA RIWAYA TEULE ZA SAID A. MOHAMED.**

Utu ni hali ya kuwa na uadilifu. Utu huhusishwa na matendo mema kama vile: kulisha, kusaidia katika shughuli, kuongoza na hata kutahadharisha wengine kiasi cha kuwaathiri vyema kisaikolojia. Ni uzuri wenye nia ya kutia wengine mazuri na mema yaliyo na kifani. Utu ni kufanya mema unavyotarajiwa na wanajamii (Oruka, 1990).

Matendo ya utu hujitokeza kwa njia mbalimbali; kwa mfano, kusaidia mayatima, maskini, wazee na wajane. Watu hawa wanaweza kusaidiwa na makao mazuri, lishe bora, nguo za kuvaa na hata elimu kwa wale wanaohitaji. Vilevile unaweza kulisha walio na njaa, kusaidia walio hatarini kama vile walionyang’anywa mali kwa njia mbalimbali, kutembelea wagonjwa hospitalini na kwa kuwasaidia kulipia ada za hospitalini na kununua dawa. Aidha unaweza kuwatembelea wafungwa ukawabebea mahitaji maalumu kama vile sabuni, sodo, mafuta ya kujipaka na mengineyo kwa kuwa pengine hukosa kuwatosha kila mfungwa kule korokoroni. Katika riwaya teule, viumbe wa kihalisiajabu wamesawiriwa wakimiliki sifa ya utu kupitia njia zifuatazo: kuonyesha upendo, kuonyesha heshima, kutoa ushauri nasaha, kusema ukweli, kuwajibikia nafasi fulani, kusamehe, kupeana motisha kwa wengine, kuwa wakarimu na hata kuwaongoza kwa njia mbalimbali.

Viumbe mbalimbali wa kiuhalisiajabu walitumia mbinu mbalimbali na hisia tofauti kuonyesha utu kwa binadamu. Hisia hizi ni kama upendo, kukosoa, kuelekeza, kutahadharisha miongoni mwa nyingine.

**Upendo**

Ni sifa mojawapo aliyo nayo binadamu. Inaaminika kuwa ilikuwepo hata dunia ilipoanza. Kwenye Biblia, Mwenyezi Mungu, kutokana na upendo alionao kwa binadamu, alitafuta Adamu na Hawa kwenye shamba la Edeni na kuwaonyesha jinsi wangefunika uchi wao baada ya wao kula tunda lililopo kwenye mti mle shambani ambalo hawakupaswa kula (Mwanzo 3:1-24). Biblia inaendelea kueleza kuwa upendo huvumilia, haujivuni, haukosi kuwa na adabu, hauhesabu

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014

mabaya, haufurahii udhalimu na huamini yote (Wakorintho wa Kwanza 13:1-12).

Mwanamke katika jamii za Kiafrika ametwikwa majukumu kadhaa yakiwemo kazi za kusafisha nyumba, kuangalia usafi wa mume na watoto na hata kupika na kuandaa chakula cha familia (Mbiti, (1991). Ingawaje ni majukumu anayopewa mwanamke, hudhihirika tu panapo upendo kwa familia. Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), upendo wa Bi. M kwa mumewe Ndi unadhihirika anapomshurutisha ale.

Anasema kuwa:

> *Leo ya tatu hujakula kitu… Unataka kujiua? Wewe mja wa ki-Islamu unafanya hivi? Unataka kujiua na unajua Mungu hawi radhi* (S. A. Mohamed 2006, p 21).

Malcolm (1959) anayeleza kuwa, ndoto ni mtiririko wa mawazo ya ndani ya mtu aliye macho au anayelala yanayoambatana na maono, taswira za matukio, mazingaombwe, fikira za uwongo, udhanifu, ndoto za mchana, ukisiaji, uwepo na malengo, matarajio na matamanio. Maelezo haya yanadhihirika wazi Ndi anapoonekana akiwa amechanganyikiwa. Hajui iwapo anaota au haoti. Ndi hana uhakika ikiwa aliuona picha ukinyanyuka au ni mwili wa Bi M. Hajui kama ni kuota anaota au ni fikira tu kutokana na athari ya video vya kutazamwa. Kisha tena anajihakikishia kuwa ni dhahiri amemwona Bi. M akinyanyuka akaemewa. Katika hali hii, utu wa Bi. M unajitokeza anapomshurutisha mumewe kula chakula. Anafanya hivi kwa kuwa siku kadhaa amejifungia tu chumbani kwake hali. Hakuwa anakula kwa sababu alikuwa na aibu kula kilicholetwa kupitia bidii ya mwanamke. Alidhani kuwa chakula kile kilipatikana kutokana na kazi ya ukahaba. Kwa kuwa anampenda mumewe, anajali afya yake na kumlazimisha kula.

**Ushauri**

Kumtolea mtu ushauri nasaha ni kumwonyesha utu. Unapotoa ushauri unaweza kuonya mtu, kumsihi afanye vitu kwa njia fulani au pia kumwelekeza katika njia mbalimbali. Kushauri mtu ni kumweleza kuhusu mambo mbalimbali anayostahili kuzingatia katika maisha yake ili ajiepushe na shida zinazoweza kumkumba katika maisha yake.

Binadamu wakati mwingine huwa mnafiki. Huweza kukudanganya tu kuhusu mengi iwapo anafaidika kutoka kwako. Unapohitaji ukweli wa kukusaidia maishani, huweza kukufichia ukweli na ukaishia kuangamia. Kwa kawaida, ukweli nao humdunga moyo binadamu kama mkuki. Mzuka hapa anamwambia K ukweli wote bila pingamizi yoyote. Mzuka, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), anamshauri K kuhusiana na mambo kadhaa. Babu, mzuka hana unafiki kama binadamu halisi. Anamshauri K kuepukana na mambo mengine. Anamwambia kuwa:

> *"Fikiri K," Sauti la mzuka sasa lilikuwa la kushawishi vya kutosha, "fikiri vipi ingekuwa kama vyakula hivi vina asili ya Kiafrika. Bila ya shaka ingekuwa hadithi ya kima na tumbili wa Zaire. Nadhani kila uzuri na ubaya wa kitu fulani katika dunia hii unatokana na msingi wa utajiri na umaskini wa watu wa asili fulani… Ukiwa na uwezo unaweza kukigeuza kitu chochote kibaya kuwa kizuri na dunia nzima itakuitikia hewalla, na tena kukufuata kuhalalisha visivyohalalishika… tena kukufwata kwa shangwe na gharama!"* (Uk 38).

Anamshauri K kuepukana na tabia ya raha na wenzake na kutumia pesa kwa vitu vyenye thamani ilhali wengine wanaumia. Anamwambia K ajijali kwa yale watakayosema watu kumhusu. K na wenzake wapo kwenye Neo-Casino. Vyakula walivyoletewa ni kama Chatu wa kutokosa, nyoka wa kukausha, kijibwa kilichochomwa miongoni mwa mengine. Mzuka anakasirishwa na mambo haya na kumzungumzia K kwa hamaki.

Babu anamwonyesha K utu kwa kumshauri kubadilisha mienendo yake. Hataki mabaya yamtendekee K. Mzuka ni mhusika wa kiuhalisiajabu ambaye ana uwezo wa kuingilia maisha ya walio hai ili kuwaonya, kuwaelekeza na kuwaelimisha. Anamkumbusha K alivyobadilika kitabia, kihadhi na kifalsafa, kwani zamani aliwachukia matajiri na kuwaita mazimwi. Mzuka anamkumbusha K alivyoahidi kutumikia raia lakini ni msahaulifu na amebadilika hivi kwamba leo ni 'msitu mpya na komba wapya '.

Kutokana na mifano iliyojitokeza, mzuka anadhihirika kuwa mfu anayetenda matendo yafanywayo tu na binadamu halisi. Mhimili mojawapo wa nadharia ya uhalisiajabu unaeleza

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014

kuwa sifa za uhalisia hukiukwa kama zilivyozoeleka. Matukio yasiyoaminika na ya kifantasia husawiriwa. Mambo ya kiajabu yanaelezwa kwa namna ya moja kwa moja kuonekana kana kwamba ni ya kawaida. Wanjiru (2013) anasema kwamba, katika jamii za Kiafrika, wazee wetu wakiwemo mababu zetu na nyanya zetu walikuwa na muda wa kukaa na wajukuu na wanao na kuwapa nasaha kuhusiana na mambo mbalimbali. Wajukuu wa kike walijiunga na nyanya zao na wa kiume wakaungana na babu zao. Inaaminika kuwa walikuwa na maarifa. Basi Mzuka, ambaye ni babu yake K, anatekeleza wajibu huo wa kutoa ushauri japo ni mfu.

### Hekima

Mwenyezi Mungu alimpa binadamu hekima. Maandiko ya Biblia katika kitabu cha Zaburi 111; 10 inaeleza kuwa, kumtii Mwenyezi Mungu ndiyo chanzo cha hekima.

Marehemu mamake Nana anatumia hekima yake kumtahadharisha Nana katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010). Anajitokeza kwa sura ya kigeni kumwonya kuhusu mwanamme. Anamweleza jinsi mwanamume ndiye kiumbe mbaya kabisa humu duniani kulingana na maneno yake yafuatayo:

> *Kwa nini hutaki kunisikia? Kwa nini enh? Kwa nini wewe huambiziki? Ni mkaidi kama babako… Unataka kuolewa, hujui kuwa kuolewa ni kudhibitiwa na mwanamume? Umetoka kwenye balaa la babako kukudhibiti kama alivyotaka kunidhibiti mimi, sasa umeingia katika mikono ya dhibiti ya mwanamume mwingine ambaye si babako wala mtu wako. Umeingia katika dhibiti ya mwanawe Faisal, wewe unamjua Faisal au huyo mwanawe? Faisal alinikimbia pale alipojua kwao. Alihalifu miadi tuliyoweka… Enh, wewe unajua nini kuhusu wanaume? Unajua nini kuhusu ndoa… ngoja mimi nikwambie* (Uk 287).

Anapojitokeza kwa sura ya kigeni, mambo huwa mabaya. Anapojitokeza kwa sura ya kienyeji mambo huwa mazuri. Anapojitokeza kwa sura ya kigeni, alimsukuma Nana, akatokatoka na kuingiaingia chumbani mwa Nana, akaanza kuhaha pumzi zikimtoka midomoni, macho yake yakawa mekundu, akasema maneno yasiyofahamika. Alisema lugha ya kuzimu. Akaanza kugwara alichokutana nacho kwa kucha zake ndefu, kisha akatoa ukwenzi wa kishetani. Alipomaliza haya, sasa angeweza kusema maneno kwa lugha inayofahamika. Mamake Nana anamwonya kuhusu mwanamme. Anamweleza alivyotawaliwa na wanaume maishani mwake na kuishia kuwachukia milele. Makumbusho haya yanaafikiana na mawazo ya (Zamora & Wendy, 1995), akieleza mojawapo ya mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu inayosema kuwa; Matukio hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Jambo hili hufanywa kwa kutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili. Mwandishi hutumia mbinu rejeshi kuvunja mtiririko wa vitushi. Utafiti hivyo umeweza kurejelea matukio rejeshi.

### Msamaha

Binadamu huhitaji kusamehe mwenzake. Katika Biblia takatifu, tunaelezewa kuwa msamaha ni kitu muhimu sana. Hata Yesu anapowafunza wanafunzi wake kuhusu maombi, anasema tuwasamehe watu kama walivyotusamehe. Biblia inatuhimiza tuweze kuwasamehe wenzetu kabla Mwenyezi Mungu hajatusamehe.

Ni jambo bora katika maisha ya binadamu, binadamu kumsamehe mwenzake. Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Dubwa anamsamehe babake kwa kutenga familia yake. Anamsamehe kwa kuona kuwa anaikimbia makusudi jukumu lake. Dubwa anamwambia;

> *Kwani hujasikia kulaumiwa wewe? Dunia nzima inakusema kwamba umeitenga nafsi yako. Kisha ukatenga nafsi ya mama watoto wako. Wanaona unajitia wendawazimu wa makusudi kukimbia dhamana na jukumu lako. Tutubu kwa Mwenyezi Mungu wetu* (Uk. 139).

Dubwa anamsihi babake atubu kwa Mwenyezi Mungu. Ili kupata msamaha, mtu hupaswa kutubu matendo yake. Hivi, naye anamsamehe babake. Ni vyema kuwa na moyo wa msamaha.

### Kutoa Msaada

Kutoa msaada ni muhali kwa binadamu. Aghalabu kila binadamu kwa wakati fulani huhitaji msaada wa mwenzake. Binadamu humnusuru mwenzake

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014

kutoka katika hali fulani akiwa amekwama. Huweza kunusuriwa kwa njia tofauti. Kwa mfano, kumsaidia mtu na hela anapofungiwa hospitalini kwa kukosa kulipa ada ya hospitalini, kumwokoa anayezama majini au hata kumwokoa jambazi kutokana na umati unaotaka kumuua.

Binadamu huhitaji msaada kwa njia mbalimbali. Vile vile, usaidizi huweza kutokea kwa kiumbe yeyote yule akiwemo binadamu au mnyama. Nyakati zingine, wanyama kama mbwa wamesikika wakisaidia kwa kutambua alipotupwa kijusi, au hata husaidia kulinda watu usiku. Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Kitoto cha miujiza kinamwonea babake huruma kwa kufungwa na kusingiziwa kuwa na wazimu bure. Anasema fika kwamba, siku moja atamkomboa babake na kila mtu. Ukombozi huu utajitokeza tu kwa kusaidiwa. Kinadhihirika hivi:

> *Wallahi' adhimu hivyo, usidhani nakizulia kimalaika cha Mungu… juzi, juzi ya kijomba, niliskia kama kinaniita- 'Mama, mama, yu wapi baba?' Nikashtuka. Kitoto cha miezi mitatu kitawezaje kusema? Kitawezaje kuuliza na kumtaka babake? Lakini usiku nilipokuwa nikilaza tena kikaongeza, "Najua baba kafungwa. Najua kasingiziwa kuua na wazimu bure, lakini mimi nitakuja kumkomboa siku moja. Nitakomboa kila mtu!"* (Uk 197).

Kitoto hapa kama binadamu pia ana hisia ya utu. Kitoto kile kinataka kumsaidia babake, ana imani ya kumkomboa babake kutoka kwenye jela ya kusingiziwa. Kila mtu pale kijijini anasema kuwa Ndi amekuwa mwendawazimu. Hii ni kwa sababu amekuwa akiishi maisha ya upweke bila familia yake. Jambo hili linaonyesha uhusiano wa dhati kati ya baba na kile kitoto. Habwe (1987) akimnukuu Kezilahabi (1976) anasema kuwa waandishi wengi wa Kiswahili hujishughulisha na utunzi wa kazi za fasihi kufuatana na matatizo au ufunuo uliowafikia wakati huo, au kufuatana na mkondo wa wakati na mabadiliko yake. Hivi ni kumaanisha kwamba mwandishi hutunga kwa kuongozwa na mambo yanayotendeka katika jamii yake wakati wa utunzi au mabadiliko yanayoikumba jamii anayoishi. Inadhihirika wazi hapa kuwa Ndi alikuwa akipata ufunuo wa utunzi wake kutoka kwa Bi Muse.

Binadamu hutafuta usaidizi kokote, kutoka kwa waganga, wanasayansi, wahubiri na hata miungu ambayo wao huamini wanaweza kuwasaidia.

**Ukarimu**

Kuwa karimu ni kuwa na tabia ya kupenda sana kutoa au kusaidia kwa hali au mali. Katika ulimwengu huu ni bayana kuwa watu hawatoshani. Kuna wale wenye uwezo kuliko wenzao. Tunapaswa tuwe wenye moyo mkunjufu ili tuweze kuwasaidia wale ambao hawajiwezi. Ingawa si kila mtu aliye na uwezo wa kupata mahitaji yake yote na kwa wingi, huwa na moyo wa kupeana. Wengine huwa wenye mioyo ya uchoyo. Ni binadamu huwa na moyo wa ukarimu. Babu Mzuka ni mkarimu. Zamora na Wendy (1995) wanaeleza kuwa matokeo ya kiajabuajabu huonekana kuwa ya kawaida.

Mwanadamu huweza kujitolea kusaidia wenzake chakula, nguo, fedha, makazi ya kuishi na kwa njia zingine mbalimbali. Babuye K, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), ambaye ni mfu aliyefufuka anajitokeza kuonyesha hisia za utu. Utu wake unajitokeza anapoonyesha upendo kwa watu maskini wanaokosa chakula ilhali K anampa mbwa wake chakula halisi wala sio hata mabaki. Anasema kuwa:

> *Niliitikiwa na ombwe, sauti yangu ikatuama huko mbali. Nilitaka kumwambia. La, nilitaka kumtanabahisha kinywa kipana kwamba sahani za vyakula anazoamrisha kuwekewa jibwa lake siku hizi naziondoa. Kwa sababu naona si halali. Nafanya hivyo kwa sababu nimejiaminisha kwamba mimi ni babu yake. Tena isitoshe, najaribu kumkumbusha K, kilembwekeza changu, kwamba wakati wetu mbwa walipewa chakula baada ya watu wote kushiba. Kwa hivyo, vyakula K anavyoamrisha vipelekewe jibwa lake, naviondosha na kuwapa majirani wanaolala njaa. Nataka kumwambia K asikasirike, kwani kufanya hivyo ni wajibu wangu…* (Uk. 2).

Utu humsukuma mtu kumsaidia mwenzake mwenye maumivu ya kimwili, kifikra na hata ya kiakili. Kwa mujibu wa Gilbert (2010) anaeleza kuwa utu una sifa za upole, unyenyekevu, maarifa na uvumilivu. Hivi kwamba, mtu aliye na sifa hizi ni rahisi awe na utu kwa wenzake. Hivyo maelezo haya yalifaa utafiti huu kwa kuwa, kutokana na upendo wa dhati alionao babu na alivyokuwa akiona watu wakijumuika kwa pamoja kusaidiana katika jamii, anawaonea huruma jirani wake ambao

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014

wanakosa chakula na kuwasaidia. Anachukua chakula cha mbwa katika hali ya kiajabu ajabu na kutoweka nacho.

## HITIMISHO

Ni suala la ajabu kwa viumbe wa kiuhalisiajabu kudhihirisha utu. Utu ni sifa ambayo huhusishwa na binadamu. Hata hivyo, sifa ya utu ilijitokeza katika viumbe hawa. Viumbe hawa wa kiuhalisiajabu walijitolea kuwasaidia binadamu kwa njia mbali mbali. Viumbe hawa wameonekana wakionyesha sifa mbalimbali za utu kwa binadamu. Sifa hizi za utu zilivyojitokeza ni kama; upendo, heshima, kutoa msaada, kuwajibika, kusamehe na mengineyo. Sifa hizi haswa zilijitokeza viumbe hawa walipokuwa wakitangamana na binadamu.

### Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu ulishughulikia kipengele cha utu wa wahusika wa kiuhalisiajabu katika riwaya teule za Said A. Mohamed. Hivyo, kutokana na utafiti huu, mtafiti anapendekeza suala la utu lipewe kipau mbele katika jamii. Kutokana na utu maisha huwa yenye upendo na Amani. Hivyo, nyenzo tofauti kama vile ufundishaji wa fasihi andishi na fasihi simulizi zitumiwe kujulisha watu kuwa sifa ya utu ni sifa muhimu katika maisha ya binadamu. Mtafiti anapendekeza pia kuwa suala la uhusika liwe suala la kushughulikiwa vilivyo katika fasihi za Kiswahili. Hii ni kwa sababu katika maisha yetu binadamu na viumbe wengine kwa wakati fulani huhusishwa na fasihi na huwa wahusika. Utafiti huu uwe kichocheo kwa watafiti wengine kushughulikia suala la utu na uhusika katika jamii.

## MAREJELEO


Chepkoech, T. (2018) "Usawiri wa maudhui yenye kufunza wanafunzi wa vyuo maadili mema: Tathmini ya Alidhani Kapata na Damu Nyeusi." (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Cornevale, J. M. (2006). *International Journal of ethics*, 16 (4), 424-429.

Cooper, B. (1998). *Magical Realism in West African Fiction.* New York: Routledge.

Danow, K. (1995). The Spirit of the Carnival; Magical Realism and the Grotesque. Kentucky University of Kentucky Press.

Gilbert, E. (2010). Magical Realism and Visionary Materialism in Okri and Blake. *Dreams of Freedom*, 15 (1), 18-32.

Habwe, J. (1987). "Euphrase Kezilahabi: Mwandishi aliyekata tamaa." Unpublished BA dissertation. University of Nairobi.

Mbatia, M. (2002). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks.

Mbiti, J. S. (1980) *The Encounter of Christian Faith and African Religion*. Retrieved 25/08/2019 On-line version published by Religion Online.

Mbiti, J. S. (1990). *African Religion and Philosophy*. Nairobi. Heinemann.

Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed S. A. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso za Mwanamke.* Nairobi: Oxford University Press.

Msokile, M. (1999). *Misingi ya Hadithi Fupi.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mwangi, J. (2013). Uhalisia na Uhalisiajabu katika Riwaya Mpya. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa)

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation Ltd

Oruka H. O. (1990). *Ethics*, Nairobi: Nairobi University.

Pietersen, H. J. (2005). Western Humanism, African Humanism and Work Organization. *SA Journal of Industrial Psychology*, 31(3), 54-61.

Samba, R. (2018) "Uhusika katika mashairi ya Kiswahili: Malenga wa Vumba, Kichomi na Utenzi wa Fumo Liyongo." (Tasnnifu ya Uzamili) Chuo Kikuu cha Maseno, Kisumu.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014

Tutu, D. (2004). *God has a Dream*: A Vision of Hope for Our Time: New York Doubleday.

Vutagwa (2013). "Sifa za uhalisiajabu katika Utenzi wa Mwana Fatuma." ( Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Wamitila, K. (2003). Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wamitila, K. W. (2010). Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi (chapa ya tano). Nairobi: Focus Publicationa Ltd.

Wanjiru, M. J. (2013). Uhalisia na Uhalisiajabu katika Riwaya za Babu Alipofufuka na Watu wa Gehhena. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Zamora, L. P. & Wendy, B. S. (1995). *Magical Realism Theory*, *History*, *Community*. London: Duke University Press.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.